



**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA VIWANDA NA BIASHARA
BODI YA USIMAMIZI WA STAKABADHI ZA GHALA**



TAARIFA KWA UMMA

Bodi ya Usimamizi wa Stakabadhi za Ghala (WRRB) imeundwa kwa mujibu wa Sheria ya Stakabadhi za Ghala (Sura 339) RE 2016. Bodi inatekeleza majukumu yake kwa mujibu wa Sheria, Kanuni na Miongozo mbalimbali iliyowekwa.

Kifungu cha 5 cha Sheria ya Stakabadhi za Ghala kinabainisha majukumu ya Bodi ikiwa ni pamoja na kutoa leseni za Mwendesha Ghala, Meneja Dhamana na Mkaguzi wa Ghala. Pia, Bodi inatoa ushauri kwa Serikali kuhusu masuala yote yanayohusiana na uendeshaji na usimamizi wa Mfumo wa Stakabadhi za Ghala nchini.

Katika msimu wa zao la korosho wa 2024/25, Bodi imetoa jumla ya leseni 35 za Mwendesha Ghala kupitia Mfumo wa Stakabadhi za Ghala kwa Mikoa ya Ruvuma, Mtwara, Lindi na Pwani.

Kufuatia mwenendo wa uzalishaji mkubwa wa zao la korosho kwa msimu wa 2024/2025 unaoendelea, imebainika uwepo wa korosho nyingi katika ghala za ngazi ya Vyama vya Msingi na Wakulima wenyewe. Katika kukabiliana na changamoto hii, Bodi imechukua hatua zifuatazo:

- i. Kuongeza leseni nyingine 4 katika Wilaya za Tunduru, Masasi, Nachingwea, Nanyumbu na Liwale ikiwa tayari Mfumo wa Kanzidata wa Bodi (WRMS) umefunguliwa kwenye maeneo hayo kwa ghala za Ushirika wa Umwagiliaji Tunduru (UMWATU), Remigio Naga, Yusra Hamza na Shamsa Feroz. Ghala hizi zina uwezo wa kuhifadhi ujazo wa jumla ya tani 1,700 kwa wakati mmoja;
- ii. Kuongeza muda wa ukomo wa kupokea mzigo ghalani kutoka saa kumi na mbili jioni hadi saa nne usiku; na
- iii. Kuongeza ukomo wa muda wa kutoa mzigo ghalani kufikia saa sita usiku.

Aidha, Waendesha Ghala wote wanatakiwa kwa haraka kuomba *extension* ya kiwango cha ujazo cha leseni zao kwa kuzingatia uwezo wa ujazo wa ghala husika pamoja na uwepo wa ghala zilizojirani ili kuongeza uwezo wa kupokea korosho ghalani.

Katika kutekeleza haya, Waendesha Ghala wanakumbushwa na kutakiwa kuendelea kuheshimu taratibu zilizowekwa na kwamba hatua kali zitachukuliwa ikibainika kwamba taratibu husika zimekiukwa.

Aidha, Bodi inawakumbusha Wanunuzi wa korosho kuharakisha utoaji wa korosho ghalani baada ya kuzinunua kwa nia ya kuongeza uwezo wa upokeaji wa mzigo ghalani.

**Imetolewa na;
MKURUGENZI MTENDAJI**